Arusha, Tanzania

Tovuti: www.african-court.org

Simu: +255-272-510-510

AfCHPR
African Court on Human and Peoples' Rights

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**TEMBO HUSSEIN**

**DHIDI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**SHAURI NA. 001/2018**

**HUKUMU KUHUSU USTAHIKI NA FIDIA**

**26 JUNI 2025**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha, tarehe 26 Juni 2025**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) imetoa hukumu katika kesi ya *Tembo Hussein dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

Tembo Hussein (Mleta Shauri) ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mjibu Shauri). Wakati wa kuwasilisha Shauri hili alikuwa gerezani akisubiri kunyongwa katika Gereza Kuu la Uyui, Tabora, baada ya kuendesha kesi, kukutwa na hatia na kuhukumiwa kifo kwa kunyongwa kwa kosa la mauaji. Mleta Shauri alidai haki zake zilikiukwa wakati wa kuendesha kesi mbele ya mahakama za kitaifa.

Mjibu Shauri alipinga mamlaka ya Mahakama pamoja na ukubalifu wa Shauri hili.

Kuhusiana na mamlaka ya Mahakama, Mjibu Shauri aliibua pingamizi kuhusu mamlaka halisi ya Mahakama. Kwa umahususi, Mjibu Shauri alihoji uwezo wa Mahakama kukaa kama mahakama ya rufaa ya jinai na kudai kwamba Mahakama hii haina mamlaka ya kufuta uamuzi wa Mahakama yake Kuu.

Kuhusiana na hoja kwamba Mahakama hii itakuwa inatekeleza mamlaka ya mahakama ya rufaa ya jinai, Mahakama ilisisitiza msimamo wake kwamba haitekelezi mamlaka ya mahakama ya rufaa kuhusiana na madai ambayo tayari yamechunguzwa

na mahakama za kitaifa. Hata hivyo, wakati huohuo, licha ya kwamba Mahakama si mahakama ya rufaa dhidi ya mahakama za nchi husika, bado ina uwezo wa kutathmini usahihi wa kesi za nchi husika endapo zimeendeshwa kinyume cha viwango vilivyowekwa katika vyombo vya kimataifa vya haki za binadamu vilivyoidhinishwa na Serikali inayohusika. Katika kutekeleza kazi iliyotajwa hapo juu, Mahakama kwa kufanya hivyo haitakuwa mahakama ya rufaa.

Kuhusu pingamizi la Mjibu Shauri kwamba Mahakama haikuwa na mamlaka ya kufuta hatia na hukumu iliyotolewa kwa Mleta Shauri na kuamuru aachiliwe huru kutoka gerezani, Mahakama ilirejelea Kifungu cha 27(1) cha Itifaki, na kuhitimisha kwamba ina mamlaka ya kutoa aina tofauti za fidia, ikiwa ni pamoja na kuachiliwa huru kutoka gerezani, ili mradi ukiukaji unaodaiwa kufanywa ulihitaji amri kama hiyo. Kwa sababu hizi, Mahakama ilitupilia mbali pingamizi lililotolewa na Mjibu Shauri.

Mahakama ilibainisha pia kwamba kulingana na kwamba ukiukaji unaodaiwa kufanywa uliwasilishwa mbele yake unahusu haki zilizowekwa katika Mkataba, ambao Mjibu Shauri ni Mhusika, ilikuwa na mamlaka ya lazima ya kushughulikia Shauri hili.

Ingawa vipengele vingine vya mamlaka yake havikupingwa na Mjibu Shauri, hata hivyo, Mahakama iliviangalia. Katika suala hili, Mahakama ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka binafsi kwani, tarehe 29 Machi 2010, Mjibu Shauri iliweka Azimio lililotolewa chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki, ambacho kinaruhusu watu binafsi kuwasilisha mashauri dhidi ya Mjibu Shauri kulingana na Kifungu cha 5(3) cha Itifaki. Mahakama ilisisitiza kwamba Mjibu Shauri kuondoa Azimio hilo, mnamo tarehe 21 Novemba 2019, hakukuathiri Shauri hili kwani uondoaji huo ulianza kutekelezwa mnamo tarehe 22 Novemba 2020, ambayo ilikuwa tarehe baada ya Shauri hili kuwasilishwa, mnamo tarehe 1 Februari 2018.

Mahakama pia iliona kwamba ilikuwa na mamlaka ya muda kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa kufanywa ulitokea baada ya Mjibu Shauri kuwa mhusika wa Itifaki. Mwisho, ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka ya kieneo, ikizingatiwa kuwa ukweli wa jambo hilo ulitokea ndani ya eneo la Mjibu Shauri.

Mahakama iliona kwamba kwa mujibu wa Kifungu cha 6(2) cha Itifaki, lazima iamue kuhusu ukubalifu wa kesi zote zilizowasilishwa mbele yake. Kuhusiana na Shauri hili, Mjibu Shauri aliibua pingamizi kuhusu ukubalifu wa Shauri hilo kulingana na kutokamilisha taratibu za ndani.

Kuhusu pingamizi la Mjibu Shauri kwamba Mleta Shauri alishindwa kukamilisha taratibu zote za ndani, Mahakama iliona kwamba Mleta Shauri alitimiza taratibu zote za ndani kwa kuwa Mahakama ya Rufaa ya Mjibu Shauri, chombo cha juu cha mahakama cha Mjibu Shauri, ilikuwa imethibitisha hatia na hukumu yake, kufuatia uendeshaji kesi ambazo inadaiwa ulikiuka haki zake. Kwa sababu hii, Mahakama ilitupilia mbali mapingamizi ya Mjibu Shauri kuhusu ukubalifu wa Shauri hili.

Mahakama iliona kwamba hakuna pingamizi lililotolewa kuhusiana na matakwa mengine ya ukubalifu, hata hivyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Mahakama, Mahakama iliangalia vigezo vyote vya ukubalifu vilivyoainishwa katika Kanuni ya 50(2) ya Kanuni za Mahakama, ambayo kimsigi inataja tena masharti ya Kifungu cha 56 cha Mkataba, ili kuhakikisha kwamba Shauri hili linatimiza viwango muhimu.

Kwa hivyo, Mahakama ilibainisha kuwa Mleta Shauri alikuwa ametambuliwa kwa udhahiri kwa jina katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(a) ya Kanuni za Mahakama. Iliona pia kwamba madai ya Mleta Shauri yalilenga kulinda haki zake kulingana na Kifungu cha 3(h) cha malengo ya Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, na hivyo Shauri hili lilitimiza Kanuni ya 50(2)(b) ya Kanuni za Mahakama.

Aidha, Mahakama ilibaini kwamba lugha iliyotumika katika Shauri husika haikuwa ya dharau au ya matusi kwa Mjibu Shauri au taasisi zake katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(c) ya Kanuni za Mahakama. Shauri hili pia halikutoka tu na habari zinazosambazwa kupitia vyombo vya habari kwani lilitokana na nyaraka za mahakama kutoka mahakama za ndani za Mjibu Shauri katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(d) ya Kanuni za Mahakama.

Kuhusiana na sharti la Shauri kuwasilishwa ndani ya wakati unaofaa, Mahakama ilibainisha kuwa uamuzi wa mwisho wa Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ulitolewa tarehe 15 Machi 2014 na Mleta Shauri aliwasilisha Shauri lake mbele ya Mahakama hii tarehe 19 Februari 2018. Mahakama pia ilibainisha kwamba Mleta Shauri aliwasilisha shauri la kupitia uamuzi wa Mahakama ya Rufaa ambalo lilitupiliwa mbali tarehe 7 Agosti 2017. Kwa hivyo, Mahakama ilibaini kuwa ufaafu wa muda wa kuwasilisha, katika suala hili, lazima uhesabiwe kuanzia tarehe ambayo Mahakama ya Rufaa ilitupilia mbali ombi la Mleta Shauri la kupitia upya uamuzi uliotolewa, yaani tarehe 7 Agosti 2017. Kwa hivyo ilibainika kuwa kipindi cha miezi sita na siku 12 ambacho alitumia Mleta Shauri kuweza kuwasilisha Shauri hili kilikuwa kinafaa kwa mujibu wa Kanuni ya 50(2)(f).

Mwisho, Mahakama ilibaini kuwa kesi hiyo haikuwa imeshughulikiwa hapo awali mbele ya mahakama nyingine ya kimataifa na kwa hivyo ilizingatia Kanuni ya 50(2)(g) ya Kanuni za Mahakama. Kwa hivyo, Mahakama ilihitimisha kwamba Shauri hili linakubalika.

Kisha Mahakama iliangalia endapo Mjibu Shauri alikiuka Kifungu cha 3, 4, 5, na 7(1)(d) cha Mkataba. Mahakama iliona kwamba hoja kuu katika Shauri hilo ilijikita katika Kifungu cha 7(1)(d) cha Mkataba, kwa hivyo, ukiukaji huu unaodaiwa kufanywa ulishughulikiwa kwanza.

Mleta Shauri alidai kwamba Mjibu Shauri alikiuka haki yake ya kusikilizwa kwa haki kwani aliona kwamba kesi dhidi yake ilikiuka moja ya kanuni za haki ya asili, ambayo ni, kanuni ya kutokuwepo upendeleo. Kwa umahususi, Mleta Shauri alidai kwamba kesi yake haikuendesha kwa haki kwa sababu inadaiwa wasaidizi wa mahakama walikuwa na upendeleo walipokuwa wakiwahoji mashahidi badala ya kuuliza maswali ambayo yalilenga kupata ufafanuzi.

Mahakama ilirejelea maamuzi yake ya awali, ambapo ilibainisha kuwa katika mfumo wa kisheria wa Mjibu Shauri, jukumu la wasaidizi wa mahakama linaishia kuuliza maswali ili kupata ufafanuzi na hawana mamlaka ya kisheria ya kuwahoji mashahidi. Mahakama ilibainisha kuwa hakuna rekodi iliyowasilishwa mbele yake inayoonyesha kwamba wasaidizi wa mahakama waliwahoji mashahidi. Mahakama pia ilibaini kwamba Mleta Shauri hakuwa ametoa uthibitisho wowote kwamba namna kesi zilivyoendeshwa mbele ya mahakama ilisababisha kosa lolote dhahiri au upotoshaji mkubwa wa haki dhidi ya Mleta Shauri. Kwa hivyo, kwa kuzingatia hili, Mahakama, ilitupilia mbali madai haya na ikaona kwamba Mjibu Shauri hakukikuka haki ya Mleta Shauri ya kusikilizwa mbele ya mahakama isiyo na upendeleo inayolindwa chini ya Kifungu cha 7(1)(d) cha Mkataba kuhusu madai ya upendeleo wa wasaidizi wa mahakama na madai kwamba waliwahoji mashahidi.

Mahakama ilibaini zaidi kwamba Mleta Shauri alikuwa ameshindwa kuthibitisha kwamba Mjibu Shauri alikiuka Kifungu cha 3 cha Mkataba. Mahakama pia ilibaini kwamba Mleta Shauri aliweza kutumia njia zote za kisheria zilizopo na kwamba aliweza kujitetea kwa mujibu wa sheria. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba hakukuwa na msingi wa kuona kulikuwa na ukiukaji na hivyo iliona kwamba Mjibu Shauri hakukiuka Kifungu cha 3 cha Mkataba.

Kutokana na kumbukumbu, Mahakama ilibainisha kwamba Mleta Shauri alihukumiwa kifo kwa kunyongwa chini ya sheria ambayo haimpi afisa wa mahakama uhuru wa kutoa uamuzi wowote, jambo ambalo hapo awali lilikuwa limeamuliwa na Mahakama



5

hii. Ingawa Mleta Shauri hakutoa maoni yoyote moja kwa moja kuhusu suala hili kuhusiana na haki ya kuishi na utu, Mahakama iliona ni muhimu kuangalia katika kesi hii mazingira yalithibitisha kuonekana suala la kutolewa adhabu ya lazima ya kifo kwa kunyongwa, kuhusiana na ukiukaji wa haki ya kuishi, inayolindwa chini ya Kifungu cha 4 cha Mkataba, na, ukiukaji wa haki ya utu, iliyohakikishwa katika Kifungu cha 5 cha Mkataba.

Katika kesi hii, Mahakama iliona kwamba Mjibu Shauri alikuwa amekiuka Kifungu cha 4 cha Mkataba, ikizingatiwa kwamba Mleta Shauri alihukumiwa kifo cha lazima chini ya sheria ambayo hairuhusu uamuzi wowote wa afisa wa mahakama kuangalia namna kosa lilivyotendeka na hali ya mkosaji. Mahakama ilisisitiza uamuzi wake katika maamuzi yake ya awali kwamba kutolewa kwa adhabu ya kifo cha lazima ni ukiukaji wa haki ya kuishi. Mahakama pia iliona kwamba Mjibu Shauri alikiuka haki ya utu ya Mleta Shauri na haki ya kutopewa adhabu ya kikatili, ya kinyama au ya kudhalilisha iliyohakikishwa chini ya Kifungu cha 5 cha Mkataba kuhusiana na njia ya utekelezaji wa adhabu ya kifo, yaani, kwa kunyongwa.

Baada ya kubaini kwamba Mjibu Shauri alikiuka haki ya kuishi na utu ya Mleta Shauri iliyohakikishwa chini ya Kifungu cha 4 na 5 cha Mkataba, Mahakama iliamuru Mjibu Shauri abatilishe hukumu ya kifo aliyohukumiwa Mleta Shauri na imwondoe kwenye gereza la wanaosubiri kunyongwa akisubiri kesi yake isikilizwe tena. Mahakama pia iliamuru Mjibu Shauri achukue hatua zote muhimu kuondoa adhabu ya kifo cha lazima kutoka kwenye sheria zake, ndani ya miezi sita baada ya kupokea taarifa ya Hukumu, na pia, achukue hatua zote muhimu ya kufanya maandalizi ya kesi ya Mleta Shauri isikilizwe tena kuhusu hukumu yake, kupitia utaratibu ambao hauruhusu kutolewa kwa hukumu ya kifo cha lazima na unaozingatia busara ya afisa wa mahakama, ndani ya mwaka mmoja baada ya kupokea taarifa ya Hukumu hii.

Mahakama pia iliamuru Mjibu Shauri aondoe "kunyonga" kwenye sheria zake kama njia ya kutekeleza hukumu ya kifo, ndani ya miezi sita baada ya kupokea taarifa ya

Hukumu hii. Mahakama pia ilimwamuru Mjibu Shauri achapishe hukumu hii kwenye tovuti za Mahakama, na Wizara ya Katiba na Sheria, ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu tarehe ya kupokea taarifa, na kuhakikisha kuwa hati ya hukumu inapatikana kwa angalau mwaka mmoja baada ya tarehe ya kuchapishwa.

Kuhusu utekelezaji wa amri hizi, Mahakama inamwamuru Mjibu Shauri awasilishe kwake, ndani ya miezi sita (6) tangu tarehe ya taarifa ya hukumu hii kutolewa, ripoti kuhusu hali ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na baada ya hapo, kila baada ya miezi sita (6) hadi Mahakama itakapoona kuwa kumekuwa na utekelezaji kamili.

Kuhusu gharama, Mahakama iliamua kwamba kila upande unapaswa kubeba gharama zake.

Jaji Rafaâ BEN Achour, Jaji Blaise TCHIKAYA na Jaji Dumisa B. NTSEBEZA walitoa Matamko yanayohusiana na kubaini kwamba Mjibu Shauri alikiuka haki ya kuishi ya Mleta Shauri inayolindwa chini ya Kifungu cha 4 cha Mkataba, kuhusiana na kutolewa kwa adhabu ya lazima, ya kifo, na kwamba Mjibu Shauri alikiuka haki ya utu ya Mleta Shauri inayolindwa chini ya Kifungu cha 5 cha Mkataba, kuhusiana na njia ya kutekeleza adhabu ya kifo, yaani, kwa kunyongwa.

**<u>Maelezo zaidi</u>**

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na hati kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, yanaweza kupatikana kwenye tovuti kupitia: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0012018

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe registrar@african-court.org

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote*



7

*cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.*



8